**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA.**

SHULE YA SEKONDARI MKULO
S.L.P 7
KIMAMBA.
.......................................

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI
.........................................................................
.........................................................................

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MKULO WILAYA YA KILOSA MKOA WA MOROGORO MWAKA ....................................**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha ............ katika shule hii mwaka .................................

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe ..............................................................

Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe ......................................na mwisho wa kuripoti ni tarehe .......................................................

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 SARE ZA SHULE

(a) Sare ya shule hii ni suruali ya kitambaa chenye rangi ya bluu bahari isiyo na mshono wa Kihuni(isibane), shati jeupe lenye mikono mifupi **(WAVULANA) – Jozi mbili.**

- Sketi ya kitambaa rangi ya bluu bahari yenye marinda **IVUKE MAGOTI** Shati jeupe lenye mikono mifupi (**WASICHANA**) – **jozi mbili.**

(b) Viatu vya shule ni vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
(c) Soksi jozi mbili nyeupe zisizokuwa na picha wala maandishi.
(d) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi
(e) Sweta rangi ya bluu kwa ajili ya kujikinga na baridi wakati wa baridi.
(f) Madaftari makubwa (counter books 10), kalamu na mkebe.
(g)Ndoo ya lita 20 na fagio kwa ajili ya usafi.

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni:-



Scanned by CamScanner

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i. Kutunza mali za shule.

## 3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

a) Wizi.
b) Uasherati na ushoga.
c) Ubakaji.
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau Bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba.
i) Kuoa au kuolewa.
j) Kutoa mimba.
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
m) Kuwa na simu ya mkononi.

## 4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Form hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Form ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu za mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MKULO

Scanned by CamScanner

SHULE YA SEKONDARI MKULO
S.L.P 7
KIMAMBA

TAREHE..............20.......

## HATI YA UTII WA SHERIA

Mimi..........................................................................
Mtoto wa Bwana/Bibi.........................................................
Mbele ya Baba/Mama/Mlezi.................................................
Nakiri kwamba nimesoma kwa makini sheria za Shule kama zilivyoandikwa katika barua yenye **Kumb.Na:MKL.S.S/ADM/VOL.**[illegible] ya Tarehe.................................
Ninazikubali sheria hizo,nitazifuata na kutii nikijua kuwa ninaelimishwa na umma kwa manufaa yangu Mimi na manufaa ya Umma.

Sahihi ya Mwanafunzi...........................

Tarehe......................

Mimi Bwana/Bibi..................................................
Mzazi/Mlezi wa ..................................................
Nimesoma kwa makini sheria za shule kama zilivyoandikwa katika barua yenye **Kumb.Na:MKL.S.S/ADM/VOL.**[illegible] ya Tarehe..................ninazikubali sheria hizo na nishiriki na uongozi wa Shule kuona kuwa Mwanangu.................................anazifuata kwa manufaa yake na manufaa ya Umma.aidha naahidi kushiriki na uongozi wa Shule katika kutekeleza m aelezo yote yatakayotolewa na Shule.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi.................................

Tarehe...............................

Scanned by CamScanner

# FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by medical Officer in a Government Hospital in respect of all new entrant to ....................................................................................................

Full Name: ....................................................................................................

1. Aids Test: ....................................................................................................
2. Blood Count (Red & White): ....................................................................................................
3. Stool Examination: ....................................................................................................
4. Urine Examination: ....................................................................................................
5. Syphilis Test: ....................................................................................................
6. T.B. Test: ....................................................................................................
7. Eye Test: ....................................................................................................
8. Ear Test: ....................................................................................................
9. Spleen: ....................................................................................................
10. Abdomen: ....................................................................................................
11. Additional information or anv other physical, mental hereditary or infections diseases:

    ....................................................................................................

    ....................................................................................................

12. Treatment after Examination:

    ....................................................................................................

    ....................................................................................................

    (Please state nature of treatment)

Medical Certificate

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to per sue further education.

Signature: ....................................................................................................

Rentination: ....................................................................................................

Station: ....................................................................................................

Official Stamp*

Scanned by CamScanner